


Head Office:
Plot 67 – 75
Clement Hill Road
KAMPALA
E-mail: exdir@unma.go.ug



Tel: +256 414 251798
Fax: +256 414 251797
P.O. Box 7025
KAMPALA
Website: www.unma.go.ug

UGANDA NATIONAL METEOROLOGICAL AUTHORITY

KISWAHILI

MAELEZO KUHUSU MFUMO WA NVUA WA KATI YA MWEZI APRIL NA MEI 2016 KOTE NCHINI UGANDA

Mfumo wa nvua ulitabiliwa kuanza katikati mwa mwezi Mechi katika sehemu kadha kote nchini. Lakini, badala yake ilitokea kuwa mfumo wa kiangazi uliendelea hadi Mechi. Baadae, nvua imeendelea kunywesha tena mapema mwezi Aprili. Kilele cha mfumo huu wa nvua kinatarajiwa kuweko katika siku za mwisho za mwezi Aprili na itakwisha katikati mwa Juni. Hata hivyo, nchi yote inatarajiwa kupata nvua ya wastani kwenye mwezi Aprili hadi mwanzoni mwa Mei.

HUU NI USHAURI SPECIALI KWA SEKTA MBALIMBALI

1. Sekta inayohusika na kilimo na kuhifadhi chakula

- Wakulima walioko kwenye sehemu nvua ilipochelewa kuanza kunywesha wanashauriwa waanze kupanda mbegu zao hivi punde.
- Utekaji maji uzidishwe kwa matuimizi ya nyumbani pamoja na yale ya nvua katika madimbwi kwa ajili ya kunyunyuzia mimea pamoja na mifugo.

- Panda nyasi za chakula cha mifugo na miti na ile ya asili itunzwe vilivyo.
- Shughuli zinazofanyika katika sehemu za miteremko zipunguzwe ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuongezeka kwa mafuriko kwa maji katika sehemu za chini.

Kwa ujumla wakulima wanashauriwa kutumia nafasi hii mvua inaponyesha sasa kwa kuzidisha mazao na kutumia ardhi vilivyo.

Kukiweko lightning

- Wenye Mamlaka katika sekta zote lazima wawahimize watu kuweka vifaa vinavyo zuia radi kwenye majengo hasa shule, hospitali na hata kwenye nyumba.
- Walimu lazima wahakikishe kwamba watoto hawachezi kwenye viwanja au chini ya miti wakati wa manyunyu ya nvua yanayotangulia kupiga radi.
- Usiguze vifaa vya chuma vinavyo weza kushika umeme unaotokana na kulipuka kwa radi.
- Jizoeze kusikiliza radio ili usikie matangazo yatakayo husu kunyesha kwa nvua na mpigo wa radi.

2. Sekta ya Miundo mbinu, Nishati na Usafiri

Nvua inayotarajiwa kunyesha inaweza kuwa nyingi na kuleta mafuriko katika sehemu nyingi. Utaratibu ufuatao lazima ufuatiliwe:

- Mamlaka ya miji lazima zizibue mitaro ilikuzia mafuliko ya maji barabarani.
- Serikali za mitaa zishirikishe wakaaji wake katika kufanya kazi za Harambee.

3. Afya

- Usafi lazima uzingatiwe nyumbani na katika shule zote.
- Zingatia mambo ya afya na toa ripoti kuhusu magonjwa kama homa ya malaria, kipindupindu, ugonjwa wa kichocho, homa ya matumbo na magonjwa mengine ya mapafu na kifua kama Athma kwa wahudumu wa Afya.

Kwa kumaliza, Kituo cha utabili wa hali ya Hewa, kitaendelea kuchunguza mabadiliko katika hali ya nga na kutoa habari na ushauri kila mara.